

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



USAJILI WA WATAHINIWA WA KUJITEGEMEA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) MEI 2019

HATUA ZA KUFUATA KATIKA KUJISAJILI KWA NJIA YA MTANDAO

1. Usajili wa Watahiniwa wa Kujitegemea **ACSEE, 2019** utanza tarehe **01/07/2018** hadi **30/09/2018** kwa kipindi cha kawaida cha usajili na tarehe **01/10/2018** hadi **31/10/2018** baada ya kipindi cha kawaida cha usajili.
2. **Malipo ya Mtihani:**
 - a) Ada ya Mtihani italipwa kabla ya kufanya usajili na itakuwa ni **Sh. 50, 000/=** iwapo italipwa kati ya tarehe **01/07/2018** hadi **30/09/2018** na **Sh. 65, 000/=** iwapo italipwa kati ya tarehe **01/10/2018** hadi **31/10/2018** ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
 - b) Malipo yote yafanywe kupitia **Posta tu** na watahiniwa wahakikishe wanapata stakabadhi za malipo vinginevyo hawatasajiliwa.
 - c) Watahiniwa ambao watafanya malipo kupitia **BENKI** mfumo hautawaruhusu kufanya usajili.
 - d) Watahiniwa wote wanasisitizwa kujisajili kwenye mtandao kabla ya tarehe **31/10/2018**.
3. **Hatua za kufuata wakati wa kujisajili:**
 - a) Fika Kituo unachotarajia kufanyia Mtihani ili kupata namba rejea (reference number). Namba hizo hutolewa bila malipo.
 - b) Unatakiwa kulipa ada ya mtihani kwa njia ya POSTA kabla ya kwenda kwenye mtandao kujisajili.
 - c) Fungua tovuti ya NECTA **www.necta.go.tz** na kisha bofya kifungo **“ACSEE 2019 PRIVATE”** upande wa kushoto.
 - d) Fanya usajili hatua kwa hatua hadi mwisho. Hakikisha unapandisha picha yako ya rangi (Passport Size) iliyopigwa kwa kutumia kamera ya digitali (digital camera) kabla au ifikapo tarehe **31/10/2018**.
 - e) Chapa nakala tatu za fomu ya kujiunga **“entry form”**.
 - f) Hifadhi nakala moja ya fomu yako ya kujiunga **“entry form”** kwa ajili ya kumbukumbu yako.
4. **Kukabidhi fomu:**

- a) Baada ya kujisajili kabidhi fomu yako POSTA uliyofanyia malipo yako ya ada kabla au ifikapo tarehe **31/10/2018**.
- b) Mtahiniwa ambaye hatawasilisha fomu yake, usajili wake utakuwa batili. Aidha Mtahiniwa ambaye atafanya malipo na kuchelewa kujisajili, hatasajiliwa kwa njia nyingine yoyote na fedha aliyolipa haitarejeshwa.

Kwa mawasiliano:

Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania, S.L.P 2624 Dar es Salaam,

Simu: 0738 78 59 45/0763 56 65 58 au 022 270493-6/9

Barua pepe; private@necta.go.tz; supports@necta.go.tz; esnecta@necta.go.tz;

Tovuti: www.necta.go.tz